

MOKASA II PRE-MOCKS 2019

KISWAHILI KIDATO CHA NNE

102/1

KISWAHILI

KARTASI YA KWANZA

INSHA

MUDA 1 ¾.

MAAGIZO

Andika Insha mbili. Swali la **Kwanza** ni la **LAZIMA**

Chagua Insha ya pili kutoka kwa maswali yaliyosalia.

Kila insha isipungue maneno 400.

Kila insha itatuzwa (alama 20)

MASWALI

1. Wewe ni katibu wa vijana katika kijii chako. Andika kumbukumbu za mkutano wenu uliojadili matatizo yanayowakumba vijana.
2. Muungano wa Afrika Mashariki una manufaa mengi. Fafanua.
3. Andika insha inayodhibitisha methali hii.....Pilipili usioila yakuashiani?
4. Andika insha inayomalizia na sentensi hii..... hili lilikuwa jambo la ajabu ambalo sikuwa nimelishuhudia maishani mwangu.

MOKASA II PRE-MOCKS 2019

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA.

KISWAHILI KARTASI YA KWANZA MUHULA WA PILI. KIDATO CHA NNE

1. Majibu yazingatie yafuatayo.
 - a. Kichwa kiwe na tarehe, mahali na wakati panapofanyika mkutano.
 - b. Waliohudhuria.
 - c. Waliokosa kuhudhuria kwa udhuru.
 - d. Waliokosa bila udhuru.
 - e. Ajenda.
 - Kusoma na kuthibitisha kwa kumbukumbu ya kwanza
 - Shughuli nyinginezo ziwe kumbukumbu ya mwisho.
 - Ajenda za mkutano wa vijana zijadili:
 - Siasa
 - Dawa za kulevyu
 - Ukosefu wa kazi
 - Usalama wa vijana vijijini
2. Manufaa ya muungano wa Afrika Mashariki.
 - a. Kuimarisha uchumi wa nchi husika
 - b. Kupanua Soko la bidhaa
 - c. Kuimarisha Mawasiliano
 - d. Umoja wa jamii
 - e. Kuimarisha usalama wa mataifa
 - f. Kuimarisha utaifa
 - g. Utangamano wa michezo.
 - h. Kudumisha uhusiano wa kidiplomasia.
3. Ni swali la methali
Abainishe maana ya methali kisha atungie kisa kinachothibitisha methali hiyo.

Maana: Jambo lisilokuhusu linakukera kiviipi au kwa njia gani?

 - Ni vyema kutoingilia mambo yasiotuhusu na yanayoweza kuleta matatizo kama vile ugomvi au vita kati ya watu wawili.
 - Akitoa kisa kisichooana na methali atakuwa amejitungia swali.
4. Kisa lazima kimalizike kwa maneno haya na kisiongezwe chochote.
 - Kisa kieleze jambo kuu la ajabu. Liwe zuri kupita kiasi au mbaya sana.
 - Kisa kioane barabara na dhamiri na maudhui yaliyokusudiwa

- Kisa kiweze kumwacha msemaji na mvuto pamoja na taharuki ili kutosheleza kimalizio.